

## **KITENGO CHA FAMASI IDARA YA AFYA.**

Kitengo cha pharmacy kipo ndani ya Idara ya Afya , kitengo hiki usimamiwa na Mfamasia wa Wilaya , akishirikiana na wataalamu wenzake. Halmashauri ya wilaya ya Ngara ina jumla ya wataalamu wa kada ya famasi 10. Wafamasia wenye shahada 2, wateknolojia dawa 5, wateknolojia wasaidizi dawa 3.

Mgawanyo wa wataalamu wa famasi ndani ya wilaya ya Ngara

Mfamasia 1 – timu ya uendeshaji wa huduma za afya wilaya(CHMT)

Mfamasia 1 na wateknolojia dawa 2 – hospitali ya Nyamiaga

Mteknolojia dawa 1 – Murusagamba kituo cha afya

Mteknolojia dawa 1 – Lukole kituo cha afya

Mteknolojia dawa 1 – Murgwanza hospitali

Mteknolojia msaidizi dawa 3 – Murgwanza hospitali

## **SHUGHULI ZINAZOFANYWA NA KITENGO CHA FAMASI NI PAMOJA NA:-**

- Kuanda mahitaji ya dawa na vifaa tiba ndani ya wilaya
- Kuunganisha taarifa na maombi ya dawa ya vituo vya kutolea huduma za afya.
- Kufanya ziara za usimamizi shirikishi katika vituo vya kutolea huduma za afya
- Kutoa elimu kwa watumishi wengine juu ya matumizi sahihi ya dawa
- Kusimamia shughuli za huduma katika Maduka ya Dawa Muhimu
- Kufanya maoteo ya dawa na vifaa tiba kwa ajili ya vituo vyote kwa mwaka.

### **Mafanikio**

1. Tumefanikiwa kuandaa na kutuma maombi ya dawa na vifaa tiba kwa ajili ya vituo kwa mwaka mzima.
2. Tumefanikiwa kuapa wataalamu 2 wa famasi kwa mwaka wa 2018 wenye viwango vya stashahada
3. Tumeendelea kutoa elimu endelevu kwa watumishi wenzetu juu ya matumizi sahihi ya dawa na shughuli za famasi kwa upana wake.
4. Kufanya ziara za usimamizi shirikishi katika vituo vya kutolea huduma za afya.
5. Tumeandaa maoteo ya dawa ya wilaya kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

### **Changamoto**

- Upungufu wa wataalamu wa famasi, kwani angalao kila kituo cha cha kutolea huduma za afya kiwe na mteknolojia msaidizi mmoja.
- Bajeti ndogo ya dawa toka serikalini kuja MSD Kwa ajili ya vituo kununulia dawa.
- Ukosefu wa baadhi ya vifaa tiba muhimu MSD eg. Catheter, haemocue cuvatte/machine
- Mlolongo mrefu wa manunuzi
- Watumishi wachache katika vituo vya kutolea huduma za afya.

### **Mapendekezo**

- Tunaomba serikali iendelee kupangia wataalama kada ya famasi kazi katika wilaya yetu
- Halmashauri iendeleo kuwa na wazabuni kwa ajili ya kufanikisha upatikanaji wa dawa/vifaa tiba zinazokosekana MSD